


MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA OKTOBA - DISEMBA, 2022 (VULI)



Dondoo muhimu za msimu wa mvua za Vuli kipindi cha Oktoba - Disemba, 2022

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa msimu wa mvua za Vuli kipindi cha Oktoba - Disemba 2022, ushauri na tahadhari kwa wadau wa sekta mbalimbali kama vile kilimo na usalama wa chakula, mifugo na uvuvi, maliasili, wanyamapori na utalii, nishati na maji, usafirishaji (nchi kavu, kwenye maji na angani), mamlaka za miji, afya pamoja na menejimenti za maafa. Utabiri huu ni mahsusini kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Nyanda za juu kaskazini mashariki, Pwani ya kaskazini, Ukanda wa Ziwa Viktoria pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma). Kwa muhtasari, mwelekeo huo na athari zake unaonesha kuwa:

a) Mvua za Vuli, 2022

- i. Mvua za Vuli zinatarajiwa kuwa za Chini ya Wastani hadi Wastani. Mvua hizo zinatarajiwa kuanza kwa kuchelewa, zenyenye mtawanyiko usioridhisha na kuambatana na vipindi virefu nya ukavu.
- ii. Mvua za Vuli zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Septemba, 2022 katika ukanda wa Ziwa Victoria. Hata hivyo, katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya nne ya mwezi Oktoba na wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2022.
- iii. Vipindi nya joto kali kuliko kawaida vinatarajiwa katika msimu wa Vuli hususani katika maeneo ya pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki.

b) Athari zinazotarajiwa

- i. Upungufu wa unyevunyevu katika udongo unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi.
- ii. Upungufu wa maji safi na salama unaweza kujitokeza na kuweza kuchocheara magonjwa ya mlipuko.
- iii. Upungufu wa malisho na maji unaweza kujitokeza hivyo kupelekea migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.
- iv. Kina cha maji katika mito na mabwawa kinatarajiwa kupungua hivyo kunaweza kupelekea upungufu wa maji kwa matumizi mbalimbali.

(I) MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA KIPINDI CHA OKTOBA - DISEMBA, 2022

Msimu wa mvua za Vuli ni mahsus kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka ambayo ni nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam na Tanga, pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kibondo na Kakonko).

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa ilivyo kwa sasa na inavyotarajiwa katika kipindi chote cha msimu (kama inavyoelezwa katika kipengele cha III cha taarifa hii), kwa ujumla mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Msimu unatarajiwa kuanza kwa kuchelewa na kuambatana na mtawanyiko wa mvua usioridhisha. Vipindi virefu zaidi vya ukavu vinatarajiwa katika miezi ya Oktoba na Novemba 2022, hata hivyo vipindi vya ongezeko kidogo la mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache hususan wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Disemba, 2022. Kwa kawaida msimu wa mvua za Vuli huisha mwezi Disemba. Hata hivyo, kunatarajiwa kuwepo na mwendelezo wa mvua kwa mwezi Januari, 2023.

Pamoja na matarajio ya mvua za chini ya wastani hadi wastani, ongezeko la joto linatarajiwa katika msimu wa Vuli hususan katika maeneo ya pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki.

1. Kanda ya Ziwa Viktoria: (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kibondo na Kakonko)):

Mvua zinatarajiwa kuwa za Chini ya Wastani hadi Wastani katika maeneo mengi ya Kanda ya Ziwa Victoria. Mvua hizi zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Septemba, 2022 katika mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara na Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma (Wilaya za Kibondo na Kakonko). Aidha, katika mikoa ya Geita, Shinyanga na Simiyu mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya nne ya mwezi Oktoba, 2022. Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Januari, 2023.


2. Ukanda wa Pwani ya Kaskazini: (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):

Mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya ukanda wa pwani ya kaskazini. Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya nne ya mwezi Oktoba na wiki

ya kwanza ya mwezi Novemba, 2022. Hata hivyo, mvua zinatarajiwa kuanza kwa kuchelewa na kuathiriwa na vipindi virefu vya ukavu. Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Januari, 2023.

3. Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki: (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):

Mvua zinatarajiwa kuwa za Chini ya Wastani hadi Wastani katika maeneo mengi ya Nyanda za juu Kaskazini Mashariki. Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya nne ya mwezi Oktoba na wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2022 na kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu, mtawanyiko na mwendelezo usioridhisha katika maeneo mengi. Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Januari, 2023.



4. Mwelekeo wa mvua za vuli katika ngazi ya Wilaya;

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imeendelea kutoa taarifa mahususi za utabiri wa msimu katika ngazi ya Wilaya. Wilaya 86 zilizo katika ukanda unaopata mvua za vuli zitapatiwa utabiri huo kwa maeneo madogo madogo. Aidha katika Wilaya hizo zote utabiri wa hali ya hewa unaonesha mvua zitakuwa za chini ya wastani hadi wastani.

Angalizo:

Ingawa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitekeza katika maeneo machache.

(II) ATHARI NA USHAURI

Taarifa ya athari na ushauri imeandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa kushirikiana na wataalamu wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika tarehe 30 Agosti, 2022.

a) KILIMO NA USALAMA WA CHAKULA

Katika msimu huu, upungufu wa unyevunyevu wa udongo unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi yanayopata mvua za Vuli. Hali hiyo inatarajiwa kuathiri shughuli za kilimo kama vile uandaaji wa mashamba, kupanda (urudiaji) na matumizi ya pembejeo za kilimo. Athari nyingine ni pamoja na ongezeko la visumbufu vya mazao kama vile mchwa, viwavijeshi, nzige na panya vinatarajiwa kujitokeza katika msimu na hivyo kuathiri uzalishaji. Wakulima wanashauriwa kupanda kwa wakati na kutumia mbegu na mazao yanayoweza kukomaa kwa muda mfupi na yanayostahimili ukame kama vile mhogo, viazi vitamu, mtama na jamii ya kunde. Wakulima wanatakiwa kuzingatia ushauri kutoka kwa maafisa ugani juu ya kanuni bora za kilimo ikiwa ni pamoja na kutumia mbinu na teknolojia za kilimo himilivu za kuhifadhi maji na unyevunyevu wa udongo na uvunaji wa maji ya mvua. Mamlaka husika zinashauriwa kutoa elimu na ushauri wa kilimo juu ya namna bora ya matumizi ya maji kwa ufanisi. Jamii inashauriwa pia kutumia chakula kwa uangalifu katika ngazi ya kaya na taifa kwa ujumla.

b) MIFUGO NA UVUVI

Upungufu wa mvua katika msimu unatarajiwa kuathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na upatikanaji wa chakula kwa ajili ya samaki. Hali hii inatarajiwa kuathiri uzalishaji wa mifugo pamoja na mazao ya mifugo na samaki. Baadhi ya magonjwa ya mifugo (yanayoenezwa na kupe pamoja na wadudu warukao) na samaki yanatarajiwa kupungua katika msimu huu. Hali kadhalika kutokana na upungufu wa malisho na maji kuna uwezekano wa migogoro kujitokeza baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Wadau wa sekta za mifugo na uvuvi wanashauriwa kuweka mipango madhubuti ya matumizi sahihi na uhifadhi wa maji na malisho ya mifugo. Aidha, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kufuatilia na kutumia taarifa sahihi za utabiri wa hali ya hewa unaotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na kuzingatia ushauri wa maafisa ugani katika maeneo yao.

c) UTALII NA WANYAMAPORI

Mvua za Chini ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa kupunguza upatikanaji wa malisho na maji hivyo kusababisha migogoro kati ya jamii zinazozunguka hifadhi na wanyamapor. Halikadhalika, milipuko ya magonjwa ya wanyamapor inatarajiwa kujitokeza kutokana na upungufu wa maji na malisho. Maambukizi ya magonjwa kutoka kwa wanyamapor kwenda kwa mifugo yanatarajiwa kujitokeza kutokana na muingiliano baina yao wakati wa kutafuta maji na malisho. Mamlaka husika zinashauriwa kutoa elimu kwa jamii iliyo katika mazingira hatarishi kuchukua hatua stahiki. Kwa upande mwingine, Jamii iliyo katika mazingira hatarishi inashauriwa kutoa taarifa kwa Mamlaka husika juu ya uvamizi wa wanyamapor katika maeneo yao.

d) USAFIRI NA USAFIRISHAJI

Sekta ya usafiri na usafirishaji ikijumuisha usafiri wa ardhini, njia ya maji na anga zinatarajiwa kunufaika kutokana na vipindi vya ukavu vinavyotarajiwa kujitokeza. Aidha, shughuli za ujenzi na maboresho ya miundombinu zinatarajiwa kunufaika katika msimu huu wa Vuli.

Hata hivyo, inashauriwa kuwa uendeshaji wa vyombo vya usafiri na mipango ya uboreshaji wa miundombinu ifanyike kwa kuzingatia taarifa za utabiri wa hali ya hewa za kila siku katika eneo husika ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

e) NISHATI, MAJI NA MADINI

Upungufu wa kina cha maji katika mito, mabwawa na hifadhi ya maji ardhini unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani. Kina cha maji katika mito na mabwawa kinatarajiwa kupungua na kuathiri upatikanaji wa maji kwa matumizi mbalimbali. Uzalishaji wa madini (hususan kwa wachimbaji wadogo) na nishati ya umeme utokanao na maji unatarajiwa kuathirika.

Watumiaji maji wanaweza kuathirika na kupelekea migogoro kati ya watumiaji wakubwa na wadogo. Hata hivyo, utekelezaji wa miradi ya umeme (hususan ujenzi), utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi unatarajiwa kuendelea vizuri. Aidha, wadau wanasisitizwa kuzingatia matumizi endelevu na kuhifadhi rasilimali maji katika shughuli za kuchakata madini, uzalishaji wa umeme, matumizi viwandani na majumbani. Halikadhalika, mamlaka husika zinashauriwa kuwa na mipango madhubuti ya uzalishaji nishati ya umeme kutoka vyanzo vingine tofauti na maji kama jua, upepo na gesi.

f) MAMLAKA ZA MIJI

Kutokana na matarajio ya upungufu wa mvua, mamlaka za miji zinashauriwa kutekeleza mipango mikakati ya marekebisho ya miundombinu ili kuboresha majengo, njia za umeme, sehemu za kukusanyia taka na mifumo ya maji safi na maji taka.

Pia, mamlaka za miji zinashauriwa kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa, kuangalia vyanzo mbadala vya maji mfano maji ya chini ya ardhi, kudhibiti matumizi ya maji holela kwa ufugaji na kilimo, kuweka miundombinu ya kuvuna maji ili kuzuia upotevu wa maji kwa matumizi endelevu ya maji.

Mamlaka za miji zinashauriwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo katika kuhakikisha usalama wa chakula, uhakika wa malisho na maji pamoja na kutoa miongozo ili kupunguza athari zitokanazo na upungufu wa mvua.

g) SEKTA YA AFYA

Hali ya upungufu wa upatikanaji wa maji safi na salama inaweza kujitokeza na kusababisha magojwa ya mlipuko katika maeneo husika kama vile vikope, magonjwa ya ngozi, kipindupindu na homa ya matumbo. Mamlaka husika zinashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari hasi, ikiwa ni pamoja na kuhimiza wananchi kutibu maji kabla ya kunywa, kusafisha matunda, kunywa maji safi, salama na ya kutosha ili kuepuka upungufu wa maji mwilini. Pamoja na hayo, mamlaka husika zinasisitizwa kutoa elimu ya afya kwa jamii ikiwemo kuzingatia usafi binafsi na usafi wa mazingira yanayowazunguka.

h) SEKTA BINAFSI

Wakulima wa mashamba makubwa wanaweza kuathirika kutokana na upungufu wa mvua ambao utasababisha matumizi makubwa ya nishati ya kumwagilia na kuhifadhi mazao tete na bidhaa. Mvua za chini ya wastani zinaweza kusababisha kuathirika kwa ubora wa miti ya nguzo na mbao.

Wadau wa Sekta binafsi wanashauriwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali ikiwemo wataalam wa hali ya hewa ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza. Taasisi za Benki na Bima zinashauriwa kuandaa na kutoa huduma mahususi kwa wadau ili kujenga ustahimilivu katika biashara.

i) MENEJIMENTI ZA MAAFA

Upungufu wa mvua unaotarajiwa utapelekea upungufu wa malisho na upatikanaji wa maji. Mamlaka husika zinashauriwa kushirikiana na kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula, malisho ya mifugo, maji na kutoa miongozo ya namna ya kukabiliana na maafa ili kuzuia na

kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Wizara za kisekta na taasisi mbalimbali zinashauriwa kuchukua hatua mahususi kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza.

j) VYOMBO VYA HABARI

Vyombo vya habari vinashauriwa kufuatilia, kupata na kusambaza taarifa sahihi za mwenendo wa msimu wa Vuli pamoja na taarifa zilizohuishwa za hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA). Wanahabari wanashauriwa kutafuta na kutumia ushauri wa kisekta kutoka kwa wataalam wa sekta mbalimbali ili kuandaa na kusambaza makala za taarifa za kisekta kwa lugha nyepesi inayoleweka na isiyoleta taharuki, kwa lengo la kuijulisha na kuielimisha jamii juu ya matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa katika kujikinga na madhara yanayoweza kujitokeza.

(III) MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la Bahari la chini ya wastani lililopo katika eneo la tropiki ya kati ya Bahari ya Pasifikasi linaashiria uwepo wa La Nina ambayo inatarjiwa kuendelea katika kipindi cha msimu wa Vuli, 2022. Kwa upande mwingine, joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) linatarajiwa kuwa la chini ya wastani wakati lile la mashariki ya Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kupunguza upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka bahari ya Hindi kuelekea maeneo ya ukanda wa Pwani wa nchi yetu na yale ya nyanda za juu Kaskazini-mashariki. Vilevile, joto la babari la juu ya wastani linatarajiwa katika eneo la kaskazini-magharibi mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kuongeza uwezekano wa kutokea migandamizo midogo ya hewa katika eneo hilo la Bahari. Mifumo hii ya joto la Bahari inatarajiwa kudhoofisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo tajwa.

Vile vile, joto la bahari la chini kidogo ya wastani katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki (nje ya pwani ya Angola) sambamba na joto la bahari la chini ya wastani katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kupelekea msukumo hafifu wa upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka misitu ya Kongo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi yetu hususan ukanda wa Ziwa Victoria.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.

Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo vitazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho ya mwelekeo wa mvua nchini kadri inavyohitajika. Aidha, wadau wanashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ili kupata taarifa mahsus za utabiri wa msimu ili kukidhi mahitaji maalum katika sekta zao.

Imetolewa tarehe: 02 Septemba, 2022

Na: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania: